HOTUBA YA MGENI RASMI MHE: HADIJAH NYEMBO MKUU WA WILAYA YA MAGU KWA AJILI YA MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI KIWILAYA KATIKA KATA YA KANDAWE WILAYA YA MAGU TAREHE 08/03/2018

Mh: Mwenyekiti wa Halmashauri,
Mh: Mkurugenzi Mtendaji wa Magu,
Wah: Madiwani,
Viongozi wa serikali,
Viongozi wa vyama vya siasa,
Viongozi wa madhehebu ya dini,
Wadau Mbalimbali wa Maendeleo,
Wataalam ngazi ya kijiji, kata na Tarafa,
Mabibi na mabwana.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani nyingi kwenu nyote mliojitokeza kuja kujumuika pamoja kwenye maadhimisho ya siku ya leo, vile vile natoa shukrani kwa wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kuweza kufanikisha maandalizi ya siku hii muhimu. Shukrani nazitoa pia kwa vikundi mbalimbali vya wanawake, ngoma, nyimbo na burudani kwa kushiriki kwenu kikamilifu, yote hayo ni katika kufanikisha maadhimisho haya.

Ndugu wananchi,

Maadhimisho ya siku ya wanawake duniani yanafanyika kila mwaka kwa kuambatana na kauli mbiu ambayo hutoa mkazo kuhusu jambo fulani. Kauli mbiu ya mwaka huu inasema“

“KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA TUIMARISHE USAWA WA JINSIA NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE VIJIJINI”. Lengo la kauli mbiu hii ni kuifanya jamii itambue kuwa msingi wa maendeleo katika jamii unachochewa

na ushiriki wa mwanamke katika uchumi kwa njia ya viwanda unaoambatana na usawa wa jinsia. Ni jambo la muhimu sana katika kumwendeleza mwanamke na kuondoa unyanyasaji, hivyo tunatakiwa kuendeleza mapambano kwa kasi zaidi na kuzidi kuhamasisha jamii ili kuamsha ari hasa wanaume waendelee kutambua kuwa wanawake ni washirika wakubwa katika suala zima la maendeleo, hivyo kwa pamoja tunaweza kujenga nchi yetu.

Ndugu wananchi,

Katika kushughulikia changamoto kama mlivyoziainisha katika risala yenu, wilaya itaimarisha masuala yafuatayo kwa lengo la kuziondoa kabisa:-

- Kuendeleza teknolojia ya uhakika wa chakula na lishe.
- Kuimarisha program za mafunzo ya lishe bora kwa wanawake, watoto na jamii kama njia ya kinga ya magonjwa nyemelezi.
- Kuongeza uelewa kwa wanawake juu ya masuala ya Jinsia
- Kuhakikisha kila familia inahifadhi chakula cha kutosha kwa matumizi na ziada.
- Kuimarisha huduma za afya na uzazi salama na kuhamasisha wanawake kupima afya zao na kujiunga kwenye mfuko wa afya ya jamii (CHF).
- Kuhakikisha wanawake wanashirikishwa katika uongozi wa ngazi zote.
- Kuhakikisha Halmashauri yetu inachangia kikamilifu katika mfuko wa maendeleo ya Wanawake na Vijana.
- Kuanzisha mtaa wa viwanda vidogo vidogo kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda vidogo (SIDO) Mwanza.

Ndugu wananchi,

Mkakati wa elimu ambao Wilaya imejiwekea ni katika kufanya jitihada za kuondoa hali ya ubaguzi wa aina zote katika jamii, sera ya elimu inahakikisha kuwa, wasichana wanapata nafasi sawa ya kuingia katika mfumo rasmi wa elimu, pia kuwawezesha kuzitumia nafasi hizo kwa ukamilifu zaidi.

Ndugu Wananchi,

Elimu ni ufunguo wa maisha. Serikali yetu imefanya juhudi kubwa katika kutoa elimu bila ubaguzi wa kijinsia. Kumekuwa na ongezeko katika uandikishaji wanafunzi katika ngazi zote tangu tupate Uhuru. Hata hivyo kiwango cha ufaulu mitihani na kuendelea na elimu ya juu kiko chini kwa wasichana ukilinganishwa na wavulana.

Hali hii inasababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo wasichana kukosa muda wa kutosha kujisomea. Hivyo ni muhimu kujenga mabweni ya kutosha kwenye sekondari zetu za kata ili wanafunzi wetu wasichana na wavulana wapate muda wa kutosha kujisomea. Aidha msukumo unahitajika ili wazazi, walezi na jamii kuelewa kuwa “Ukimuelimisha msichana umeelimisha familia na Jamii kwa ujumla”.

Jamii pamoja na wadau mbalimbali wa elimu tushirikiane na serikali yetu kutoa michango mbalimbali ya hali na mali kufanikisha ujenzi wa mabweni na maabara za kutosha katika shule zetu za sekondari za kata ili kuboresha elimu.

Ndugu wananchi,

Tunatakiwa kuboresha elimu ya mtoto wa kike na kuhakikisha kwamba idadi ya watoto wa kike wanaopata elimu ya sekondari na vyuo vikuu inaongezeka. Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla tuwajibike kuwafundisha watoto wa kike na kiume maadili mema.

Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, wahisani na taasisi nyingine ziendelee kushirikiana kwa pamoja katika kutetea na kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia. Tupige vita rushwa katika sehemu zetu za kazi, ili kuboresha maadili ya kazi na ufanisi zaidi.

Tuendelee kutoa mafunzo na ushauri mbalimbali ili kuwawezesha wanawake kuendesha shughuli zao katika ajira isiyo rasmi kwa ufanisi. Kuhamasisha na kuelimisha wanawake na jamii kwa ujumla kuhusu haki za kisheria zinazowagusa wanawake, mfano umiliki wa ardhi kama rasilimali ya msingi katika kilimo, ufugajina uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo.

Tunatakiwa kuongeza juhudi za utoaji elimu kuhusu faida na njia za uzazi wa mpango na afya ya uzazi kwa ujumla na pia kujikinga na maambukizi ya VVU UKIMWI. Aidha natoa wito kwa wanaume waone umuhimu wakushiriki kikamilifu katika masuala ya afya ya uzazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kutokana na ushiriki wao kuonekana kuwa mdogo kwa sasa.

Ndugu wananchi,

Kundi la wanawake lina mchango mkubwa katika Maendeleo ya Jamii,hata hivyo Serikali kwa upande wake imeendelea kuwawezesha wanawake kupitia vikundi vya ujasiriamali kwa kutumia mfuko wa maendeleo ya wanawake. Ambapo kwa mwaka 2017/2018 wanawake wapatao 160 wamenufaika na mkopo wenye thamani ya Tsh. 32,000,000.00 umetolewa kwa vikundi 32 vya wanawake.Nachukua fursa hii kuwasisitiza wanawake wanaopata mikopo warejeshe kwa wakati ili mikopo iendelee kutolewa kwa wanawake wengine.

Maendeleo ni yetu sote hivyo basi, ili kuinua vipato vya wananchi katika wilaya yetu natoa wito kufanyika kwa mambo yafuatayo:-

- Wananchi wote wanawake kwa wanaume waelimishwe na kusaidiwa kutumia fursa zilizopo za kuinua kipato kupitia biashara, kilimo, mifugo na Uvuvi.

- Wananchi wote waelimishwe kuhusu matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi katika uzalishaji.
- Zitumike mbinu zenye ufanisi za kuelimisha na kuraghabisha jamii kwa masuala mbalimbali.
- Wananchi waelimishwe stadi za ujasiriamali, ufundi na uongozi katika shughuli za kiuchumi.
- Wananchi waelimishwe na kusaidiwa kuanzisha mitandao ya habari kwa kupata ajira na mafunzo
- Wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa wanaume na wanawake, hasa wenye wenza kushirikiana katika shughuli za kuinua vipato vya familia zao.

Ndugu wananchi,

Wilaya yetu ni moja ya wilaya zinazofanya jitihada za kuhakikisha wanawake wanachukua angalau nusu ya nafasi zilizopo kwenye vyombo vya maamuzi. Katika kipindi hiki wanawake wamejitokeza kugombea uongozi mbalimbali na kufanikiwa kupata nafasi zifuatazo: Wenyekiti wa vitongoji wanawake 7, wajumbe wa halmashauri za vijiji wanawake 607, madiwani wa kuchaguliwa mwanamke mmoja na madiwani wanawake wakuteuliwa 8.

Ninawaasa wanawake wote mzidi kuomba nafasi katika ngazi mbali mbali za maamuzi. Pia tuzidi kuihamasisha jamii nzima izidi kuwaamini wanawake na kuwapa nafasi katika nafasi mbali mbali za uongozi.

Ndugu Wananchi,

Maendeleo ndani ya wilaya yetu yanaletwa kwa ushirikiano kati ya wanawake, wanaume, serikali na wadau mbalimbali.

MWISHO: Nimefurahishwa sana kwa kushiriki kwenu kikamilifu, nina kila sababu ya kushukuru kwa ushirikiano wenu. **"KUELEKEA UCHUMI WA VIWANDA TUIMARISHE USAWA WA JINSIA NA UWEZESHAJI WA WANAWAKE VIJIJINI".**

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.